Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Vipengele Vya Ontolojia Katika Tamthiliya Za Kiswahili: *Mashetani* (1971) Na *Kivuli Kinaishi* (1990).

**Rosalina Karata[1]; Dr. Muusya Justus[2]; Dr. Rose Mavisi[3].**
**[1.2.3] Catholic University of Eastern Africa.**
**[2.3] justusmuusya1982@gmail.com; rosemasai@gmail.com**
**Main Author Email: karatarosa@gmail.com**

## IKISIRI

Makala haya yalilenga kuchambua vipengele vya Ontolojia ya Kiafrika katika tamthiliya za Kiswahili: mfano wa *Mashetani (1971)* na *Kivuli Kinaishi* (1990). Mbinu iliyotumika katika kukusanya data hii ni mbinu ya kitaamuli. Sampuli iliyotumika katika makala haya ni vitabu viwili vya tamthiliya ambavyo ni *Mashetani* (1971) na *Kivuli Kinaishi* (1990). Tamthiliya hizi zitawakilisha zingine nyingi ambazo zimeandikwa na Ibrahimu Hussein na Said Mohamed. Mtafiti atajikita katika tamthiliya hizo mbili ili kuchambua vipengele vya ontolojia. Utafiti huu ulifanywa maktabani ambapo data ziliweza kukusanywa kwa kutumia mbinu ya udurusu maktaba. Mtafiti alipitia maandishi mbalimbali kutoka katika vitabu vilivyopo katika maktaba pamoja na wavuti ili kupata maelezo yaliyotosha kukidhi haja ya makala haya. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ambapo mtafiti aliitumia katika kuchambua vipengele vya ontolojia ya Kiafrika katika tamthiliya teule. Makala haya yatasaidia kuongeza uelewa kwa wanajamii hasa kwa wale wasiofahamu kuchambua masuala ya kiontolojia katika fasihi andishi. Kutokana na matokeo ya utafiti huu tumefikia mahitimisho kuwa vipengele vya ontolojia ya Kiafrika vilivyobainishwa kutoka katika tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* vimeweza kusawiri ontolojia ya Kiafrika na nafasi yake kwa jamii.

**Maneno muhimu**: Ontolojia, tamthiliya, kitaamuli, Mashetani, Kivuli Kinaishi.

---------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA.**

Karata, R., Muusya, J. & Mavisi, R. (2021). Vipengele Vya Ontolojia Katik a Tamthiliya Za Kiswahili: *Mashetani* (1971) Na *Kivuli Kinaishi* (1990). *Editon Cons. J. Kiswahili,* 3(1), 293-306. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v3i1.268

---------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
ISSN: 2663-9289
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**UTANGULIZI**

Dhana "Ontolojia" inatokana na neno la Kigiriki "ontos" lenye maana ya "kuwako" na logos lenye maana ya "sayansi" inayohusiana na maarifa ya metafizikia (Stumph na Fierser, 2008). Heidegger (1999) anaeleza kuwa, Ontolojia ni elimu inayohusika na ardhi, anga, wanadamu na miungu, na hivyo kumfanya mwanadamu kuwa na upeo wa juu wa kuelewa mazingira yake. Ontolojia ni dhana inayojishughulisha na asili ya uhai na inatumika kuelezea hali ya kuwako kwa kitu (Wamitila, 2003).

Ontolojia ni mtazamo mpana katika dunia unaoangalia vitu katika uhalisia wake kutokana na kuwa dhana hii imepitia mikondo mbalimbali ya mabadiliko na mitazamo, hivyo kuifanya kuwa na historia yake (Roe, 2012). Hata hivyo, ni vigumu kubaini tarehe rasmia ambayo Ontolojia ilianza. Chanzo chake kwa kiasi kikubwa kinahusishwa na hali ya maarifa ambayo binadamu huyatumia katika kukabiliana na mazingira yake. Ontolojia ni tawi la metafizikia katika taaluma ya falsafa linalochunguza dhana ya uwepo na kuwepo (Smith, 2003). Ontolojia ni mwongozo unaoelekeza jamii kwa kuwa hujikita katika kuwapo na kuacha athari kubwa kwa wanajamii. Ontolojia ni maarifa mbalimbali yanayotoka katika taaluma za falsafa na sayansi ili kutatua matatizo yanayojitokeza katika jamii.

Baadhi ya wataalamu kama vile Mbiti (1969) anabainisha vipengele vya Ontolojia ya Kiafrika kuwa ni dhana ya wakati, kuwapo kwa Mungu mkuu, kuwapo kwa mizimu, familia pana, kifo, ndoa na uzazi, matambiko na utoaji wa majina kwa watoto. Naye Kezilahabi (1985) na Nyanto (2016) wanabainisha vipengele vifuatavyo vya Ontolojia ya Kiafrika: Miiko, uchawi, miungu, uduara wa maisha ya mwanadamu, kifo na maisha baada ya kifo, roho kuhama kutoka kiumbe kimoja kwenda kiumbe kingine, kuwapo kwa mizimu na matambiko. Vipengele hivyo vilivyobainishwa na wataalamu ni vya msingi sana na vimeweza kutupa picha ya kuweza kuvibainisha vipengele vya Ontolojia ya Kiafrika kutoka katika tamthiliya teule. Makala haya yanalenga kubainisha ikiwa kuna vipengele vya Ontolojia katika tamthiliya ya *Mashetani* (1971) na *Kivuli Kinaishi* (1990).

**Mapitio ya Maandishi**

Tamthiliya zilizotumiwa katika utafiti wetu ziliweza kutafitiwa awali. Salem (2013), alifanya utafiti linganishi wa tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* kwa kutumia mkabala wa kiulinganishi. Lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza ulinganifu na utofauti uliopo kati ya tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* na sababu zilizofanya tamthiliya hizo zifanane au zitofautiane kimaudhui na kifani. Utafiti huo ulimpatia mtafiti uelewa wa namna ya kufikia malengo yake. Hii ni kwa sababu alichunguza tamthiliya mbili za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi.* Tamthiliya hizi ni baadhi ya kazi zilizotafitiwa katika utafiti huu. Pamoja na kulingana huko, kazi ya Salem ni tofauti na kazi hii kwa sababu utafiti huu ulilenga kufanya uchunguzi wa vipengele vya Ontolojia ya Kiafrika katika tamthiliya za Kiswahili katika kuchanganua matini za kifasihi kwa kutumia nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika katika tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*.

Chuachua (2016) ambaye alitafiti falsafa ya riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika muktadha wa epistemolojia ya Kibantu. Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu imechunguza namna maarifa ya Wabantu yanavyojitokeza katika riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Uchunguzi huo umezingatia vipengele mbalimbali kama vile uchawi, tambiko, imani au fikra zao kuhusu roho na kifo, moyo, Mungu, uzazi, utoaji majina, uganga na ardhi. Utafiti huu utatusaidia katika kudhihirisha kuwa Waafrika wana namna yao ya kupata maarifa ambayo ni kupitia kani-uhai toka kwa Mungu wao. Wazee walio hai ndiyo chanzo cha



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

maarifa hapa duniani kwa kuwa wana uwezo wa kuwasiliana na wahenga wao kwa urahisi zaidi. Aidha, kujua kwao kumefungwa kwenye duara linalofanywa na kani-uhai toka kwa Mungu, kuja kwa wahenga, kisha kwa watu walio hai na kurudi tena kwa Mungu. Mungu ndiye chanzo kikuu cha kani-uhai. Aliye nje ya duara hili linaloundwa na kani-uhai, hawezi kuwa na maarifa ya kuhusu jamii yake. Kwa Waafrika, maarifa ni kujua asili ya kani-uhai na athari zake. Jambo hili hutokana na uzoefu wa muda mrefu wa kaida za jamii husika; pamoja na kudumisha mila na desturi zinazoimarisha uhusiano uliopo ndani ya duara la maisha. Utafiti umebaini kuwa maarifa ya Waafrika yanaegemea katika misingi ya kiontolojia na katika kudhihirisha hili, vigezo vinavyotumiwa na Waafrika katika kumbainisha mtu vimewekwa bayana. Hivyo, utafiti wa Chuachua ulitusaidia kuwekea utafiti wetu msingi bora katika kubaini vipengele vya ontolojia kutoka katika matini teule.

**Nadharia ya Ontolojia**

Ontolojia ya Kiafrika ni tawi la metafizikia linalohusiana na maumbile na uhusiano wake na kuwako Mbiti (1969). Ontolojia ya Kiafrika ni mtazamo wa Wawaafrika kuhusu maisha, kuwako kwa binadamu na ulimwengu kwa ujumla. Ontolojia ya Kiafrika hurejelea umoja na mshikamano wetu ambao hauwezi kuharibika wala kuvunjika. Kwa mfano: - imani za jamii kuhusu maisha, mwanadamu na ulimwengu. Umoja na mshikamano ni msingi mkuu kwa Waafrika.

Tempels (1959) anaeleza kuwa, falsafa ya Kiafrika kwa kiwango kikubwa inazungumzia Ontolojia ya Kiafrika licha ya Waafrika kutamalaki maeneo mengi duniani. Waafrika kwa asili wana mambo mengi ambayo ni ya asili na ili tuweze kuyafahamu ni lazima tutumie Ontolojia katika kuyachambua. Maisha ya Waafrika yamejikita katika misingi inayowaongoza. Pia wana namna yao ya kutatua matatizo yanayowapata. Mfano, kuhusisha wahenga katika kutatua matatizo. Hata wale walioingia katika dini za kigeni hulazimika kurudi katika dini za asili au jadi pindi wanapopatwa na matatizo. Waafrika wana misingi yao ya kuheshimu wahenga. Waafrika wanaamini kuwa wanaongozwa na nguvu fulani ambayo imepangwa kidarajia.

i. Mungu muumbaji – aliyeweka kuwako, ambaye ndiye hutawala nguvu nyingine zote.
ii. Waasisi wa ukoo na miungu – mungu huwasiliana nao kwa nguvu maalumu ili kuendeleza ulimwengu.
iii. Watu wa kawaida wale ambao wanaishi.

Falsafa ya Kiafrika ina misingi yake ndani na nje ya kuzimu. Mbiti (ameshatajwa) anaeleza kuwa, maisha ya kawaida ya Waafrika yamekaa pia kidarajia na hii hufikiwa baada ya kuoa au kuolewa na ukamilifu wake hutokea baada ya wanandoa kupata watoto. Ugumba hufikiriwa kuwa ni laana mbaya sana kwa kuwa mgumba hatakumbukwa baada ya kifo chake. Akifafanua mduara wa uzazi, majira na kifo anaeleza kwamba, mtu hafariki bali huzaliwa kupitia jina la mtu mwingine. Aidha, dhana ya kifo na uzazi inatupa dhana nyingine ya wakati ambapo mtu anapofariki mwili huachana na roho lakini mtu huyo huendelea kuishi endapo tu jina lake limechukuliwa na mtu mwingine lakini kama halijachukuliwa basi mtu huyo haishi tena. Ndio maana katika jamii za Kiafrika kuna utamaduni wa kurithishana majina ambapo mtoto anapozaliwa hupewa jina la babu, bibi, mjomba, shangazi, na kadhalika kwa lengo la kuendelea kumkumbuka. Licha ya hayo, kwa Waafrika jina limefumbata maana ya nje na ya ndani. Maana ya nje huhusishwa zaidi na hali, wakati na mazingira, na maana ya ndani huhusishwa na hulka, tabia na matendo ya mhusika. Mambo yanayojitokeza katika usawiri wa Ontolojia ya Kiafrika ni Mungu na uwezo wake, mizimu na nguvu zao katika kuwasaidia wanadamu, uzazi na malezi, utu, heshima kwa wakubwa, imani za uchawi, uganga na sihiri.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
ISSN: 2663-9289
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Nadharia ya Ontolojia hujumuisha maisha, mazingira pamoja na fikra za watu. Mawazo ya Mwafrika hujengwa katika misingi ya nguvu mbalimbali ambazo ni miungu, binadamu, mimea na kadhalika. Mawazo haya yamejenga nadharia inayomuongoza binadamu juu ya ufahamu wa misingi hiyo ya nguvu mbalimbali zinazosababisha kuwepo. Nadharia hii ni zao la muda mrefu linalotokana na uzoefu walionao watu pamoja na hisi. Uzoefu huu na hisi huangalia msingi wa utokeaji na mwonekano wa vitu katika darajia zake na kuonyesha vipengele mbalimbali vya Ontolojia ya Kiafrika.

**Matokeo**

**Vipengele vya Ontolojia katika Tamthiliya ya *Mashetani***

Utoshelevu wa vipengele vya Ontolojia ya Kiafrika katika tamthiliya ya *Mashetani* (1971) ulikuwa sehemu muhimu ya makala haya. Utafiti wetu ulibaini kuwa tamthiliya teule zimebeba utajiri mkubwa wa vipengele vya Ontolojia ya Kiafrika. Hii ni kutokana na taarifa zilizopatikana katika udurusu wa maandiko mbalimbali maktabani.

**i. *Tiba za jadi***

Kulingana na nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika kipengele cha tiba za jadi kimeweza kusawiriwa katika tamthiliya teule. Waafrika wanaamini kuwa Mungu aliyewawezesha kuwapo huwapa uwezo wa kuweza kugundua dawa za jadi ambapo wanapozitumia huwaletea uponyaji katika maisha yao. Mbogo (2008) anaeleza kuwa, tiba za kijadi huweza kuleta madhara kwa baadhi ya watu kama zitatumiwa vibaya, lakini zaweza kuwa suluhisho kubwa la matatizo ya binadamu kama zitatumiwa vizuri.

Waafrika wanaamini sana tiba za jadi kama kipengele cha Ontolojia ya Kiafrika kwa sababu ndizo zinazoweza kutatua baadhi ya matatizo yao ambayo yameshindikana kupata ufumbuzi kupitia njia za kisasa (hospitalini) zitumikazo katika jamii. Dai hili linadhihirika baada ya Kitaru kupatiwa matibabu kutoka kwa madaktari wa hospitali za kisasa bila kuonyesha matumaini ya kupona, ndipo suluhisho pekee lililobakia ni kuanza kuzigeukia tiba za jadi. Nukuu ifuatayo inadhihirisha dai hili;

> **Mama:** *Afadhali tutafute dawa za kienyeji basi. Imekuwa dawa za kizungu hazifai. Sasa tufanyeje?*
> **Baba:** *Aliyesema hazifai nani?*
> **Mama:** *Acha kujikurupusha bwana. Sasa tunamwita mganga au Hatumwiti?...* (uk. 30-31).

Katika nukuu iliyo hapo juu inaonyesha kuwa, baba yake Kitaru alionyesha kuwa na imani na madaktari wa hospitali za kisasa lakini mke wake hakuwa na imani kabisa na dawa za hospitalini. Aidha, kitendo cha baba Kitaru kumkubalia mkewe kumwita mganga wa kienyeji kinaonyesha kuwa baba Kitaru anaukubali uzuri wa tiba za kijadi. Hivyo, tiba za jadi katika jamii za Kiafrika zina thamani na uzuri maridhawa kwa sababu wanaamini kuwa, zitawasaidia katika kutatua matatizo ambayo yameshindikana kutatuliwa kwa njia za kisasa yaani hospitali.

**ii. *Matumizi ya Nyimbo***

Nyimbo ni kipengele kimojawapo katika nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika chenye kubeba dhima tofauti tofauti katika jamii. Waafrika wanaamini kuwa kipaji cha kutunga nyimbo kinatoka kwa Mungu na kumpatia mwanadamu ili aweze kukitumia katika shughuli zake mbalimbali. Nyimbo ni sanaa ya maonyesho inayowasilishwa kwa kutumia mitindo ya utendaji wa kimuziki (Omari, 2009). Katika jamii za Kiafrika nyimbo ziliimbwa katika matukio mbalimbali kama vile harusi, matambiko, misiba na sherehe za mwaka. Watendaji hufanya hivyo kwa lengo la kufurahisha au kuliwaza jamii kwa kuwa wanao uwezo waliopewa na Mungu wa kutunga na kuwasilisha sanaa yao papo kwa papo bila maandalizi yoyote. Katika tamthiliya hii nyimbo zimeweza kubainika katika nukuu ifuatayo;

> **Baba Kitaru:** *(anaimba)*
> *Papa pa papapa*



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
ISSN: 2663-9289
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

> *I like some m … (uk. 21-22).*

Wimbo huo unaonyesha furaha aliyokuwanayo baba Kitaru baada ya kununua gari aina ya Benz na alipofika nyumbani kwake alishirikisha furaha hiyo katika familia yake. Pia katika uk. 09-10 Binadamu anaimba kufurahia ushindi baada ya kumuua Shetani. Hali hii inaonyesha kuwa, jamii za Kiafrika zinapofanikiwa jambo fulani katika maisha hufurahi kwa kuimba na kucheza kwa furaha.

**iii. *Matumizi ya Misingi ya Uduara***

Kipengele kingine cha Ontolojia ya Kiafrika kilichosawiriwa katika tamthiliya ya *Mashetani* ni matumizi ya misingi ya uduara. Uduara ni jambo linalotiliwa maanani sana na jamii za Kiafrika, wanaamini kuwa jambo linapofanywa katika duara huwa limekamilika. Kiango (1973) anaunga mkono hoja hii kwa kueleza kuwa, kwa Waafrika, ngoma ilichezwa na kila mmoja aliyehitaji kucheza. Hivyo kutokana na uzuri huu, Waafrika wanapenda kucheza ngoma zao na kutenda mambo mbalimbali kwa sura ya duara. Duwe (2016), yeye anaeleza kuwa matumizi ya duara ni pamoja na kurahisha jambo kwa kulifanya kwa ushirikiano ili kumfanya kila mwanajamii anayehitaji kushiriki katika jambo fulani kushiriki kwa urahisi bila taabu yoyote. Mambo ambayo hufanywa kwa kuzingatia misingi ya uduara katika jamii za Kiafrika ni shughuli za huzuni na furaha. Katika tamthiliya hii dhana ya uduara imejitokeza katika kusherekea ushindi kwa kucheza na kuimba kwa Binadamu (Kitaru) anapofurahia kumuua Shetani (Juma). Furaha yake inakamilika katika kuizunguka maiti na kuifanya kuwa katika duara la uwanja wa kusherekea. Binadamu anasema:

> *(Anapiga vigelegele kwa furaha. Anaruka ruka na kuizunguka maiti kwa furaha kubwa. Anacheka mpaka michozi inamtoka. Anacheka mpaka furaha na kicheko vinamlevya. Anauendea ule mbuyu kwa haraka na huku anacheka. Anaimba).*
>
> *Wako wapi waliokuwa wakijitapa?… (uk. 09).*

Kitendo cha binadamu (Kitaru) kusherehekea kwa kuizunguka maiti ni tajiriba za Mwafrika. Uduara ni kipengele muhimu sana katika maisha ya Waafrika kwa sababu furaha yake inatimia kwa kucheza kama ishara ya kufurahi na kusherekea kwa kuunda umbo la duara. Duara hili huwafanya wanaocheza waweze kuonana na kuitikia kiitikio cha wimbo unaoimbwa kwa urahisi.

**iv. *Matumizi ya Mapango na Mibuyu***

Mapango na mibuyu ni vipengele vya ontolojia ya Kiafrika vilivyoweza kubainishwa na mtafiti katika tamthiliya ya *Mashetani*. Vipengele hivi vinaipa tamthiliya teule uzuri katika uelezaji wa matukio mbalimbali yanayotendeka katika jamii. (BAKIZA, 2010) anaeleza kuwa mbuyu ni mti mkubwa wenye kivimba kinene unaozaa matunda yenye gamba gumu na kokwa nyingi. Aidha, kwa mujibu wa nadharia ya Ontolojia, inalenga kuifungamanisha kazi hii na mazingira ya Kiafrika ambapo Waafrika wanaamini kuwa mapango na mibuyu hutumika katika shughuli mbalimbali kama vile kutolea sadaka kwa miungu na sehemu ambayo mashetani wanaishi. Katika kuonyesha matumizi ya mapango na mibuyu, mwandishi anasema.

> **Juma:** *Wananchi; kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma na rafiki yangu Kitaru, tutakuonyesheni mchezo wa Shetani na Bidanamu. Mimi nitakuwa Shetani, na Kitaru, atakuwa Binadamu. (Mbio, Juma anaingia katika pango la mbuyu. Anakaa kwa muda mrefu) (uk.01).*

Mti wa mbuyu unapoota mahali popote huwa ni sehemu ya kazi ambapo mambo mbalimbali yanatendeka yakiwemo matambiko, uganga na uchawi. Aidha, katika karne nyingi zilizopita Ontolojia ya Kiafrika ilieleza kuwa mbuyu ni mti wa baraka, ni mti unaobeba nguvu za kutatua matatizo ya jamii. Kutokana na tukio la Kitaru kuumwa kichwa baada ya kushiriki mchezo uliochezwa baina yake na Juma, mbuyu unabatizwa na jamii kuwa shetani anawachulia. Pango lililopo katika mbuyu linakuwa sehemu inayotisha na kusababisha mgogoro kati ya Juma na Kitaru. Katika jamii nyingi za Waafrika



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

wanaamini kuwa sehemu yenye pango ni makazi ya shetani, mizimu, mazimwi na baadhi yao hutumia sehemu hiyo kwa ajili ya shughuli za uganga.

**v. *Suala la Uzazi.***

Waafrika huchukulia suala la uzazi kama jambo muhimu katika jamii. Mtu mwenye uzazi huonekana wa thamani na asiye na uzazi huchukuliwa kuwa ni mtu aliyelaaniwa na Mungu na asiye na thamani yeyote katika jamii yake. (Geofrey, 1969; Kajosi, 2013 na Chuachua 2016). Kipengele hiki ni chamsingi sana kwa jamii za Waafrika ambapo ni tofauti na maelekeo ya watu wa magharibi ambao hawaangalii suala la uzazi kama la muhimu na lenye manufaa kwao. Katika jamii za Waafrika kuwa na wake wengi ni tendo la ufahari, hali ambayo huhusishwa na uzuri uwezeshao wake hao kupata watoto wengi ili kupanua familia na ukoo kwa ujumla. Aidha, kwa Waafrika, ndoa ambayo haina uwezo wa kupata watoto ni rahisi sana kuvunjika kwa sababu watoto ni hazina ya baadaye na walezi wa wazazi hao wakati wa uzee. Katika tamthiliya hii mtafiti ameweza kubaini suala la uzazi kama kipengele muhimu cha Ontolojia kwa Waafrika. Wahusika katika tamthiliya hii wamesawiriwa wakiona fahari kuwa na watoto kama (Mbiti, 1969) anavyoeleza kuwa, kupata watoto ni baraka na kinyume chake ni laana. Hili linathibitika katika nukuu ifuatayo:

> **Shetani:** *Rafiki mpenzi, rafiki mwandani. Rafiki wa milele, rafiki wa daima. Ninakupokea. Ninaifurahikia leo, siku ya uzao wako. Kutoka katika tumbo la giza jeusi, kuingia katika ulimwengu wa nuru nyeupe. (uk. 04).*

Maelezo haya yanaonyesha namna hali ya kuwa na watoto ilivyo jambo muhimu kwa Waafrika. Ndiyo maana mwandishi anasisitiza kuwa kinachozaliwa huwa ni kizuri kuliko kinachozaa kwa sababu mtoto katika jamii za Waafrika ni baraka na sio laana.

**vi. *Suala la Umoja***

Umoja ni kipengele muhimu katika nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika ambacho hutambulisha tabia ya Kiafrika. Kulingana na Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015) inafasili umoja kuwa ni hali ya kushirikiana katika kufanya jambo. Jamii za Waafrika zimejengwa katika utamaduni wa kuishi kwa umoja. Umoja huu huwa katika mambo ya furaha na ya huzuni. Hoja hii inashadidiwa na Mbiti (2011:108-109) anaposema:

> *Katika maisha ya kijadi ya Waafrika, mtu hawezi kuishi peke yake, bali kwa ushirika pamoja na wenzake. Kuwapo kwake kunategemea wengine, wakiwemo wale wa vizazi vilivyopita na wale wa wakati wake kwa kuwa yeye ni sehemu tu ya jamii nzima. Kwa hiyo, jamii haina budi kumtengeneza, kumuumba na kumfunza mtu kwa kuwa mtu huitegemea jamii anayoshirikiana nayo... Atesekapo, hateseki peke yake, bali pamoja na jamii yake. Afurahiapo, hafurahi peke yake bali pamoja na ndugu zake ... (TY).*

Kwa maana hiyo, katika mhimili wa kwanza katika nadharia ya Ontolojia Waafrika wanaamini kuwa Mungu muumbaji ndiye anayewawezesha watu kufanya mambo mbalimbali kwa pamoja ili kuweza kuleta maendeleo. Katika jamii za Kiafrika mtu hawezi kufanya jambo peke yake na kupata mafanikio. Dai hili linashadidiwa na nukuu ifuatayo;

> **Kitaru**: *Kitendo cha kila siku, maisha ya kila siku yanabadilishwa na watu.*
>
> **Juma**: *Lakini siyo vijitu viwili. Kwa heri (uk. 57).*

Maelezo haya yanaonyesha umuhimu wa umoja katika kuleta maendeleo na kuondoa matatizo yaliyomo katika jamii. Hapa mwandishi anaonyesha kuwa maisha yanabadilishwa na watu na sio watu wawili peke yao, hivyo watu wakifanya shughuli mbalimbali kwa kushirikiana hakuna jambo lolote linaweza kushindikana kwani umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

**vii. *Suala la Adabu***

Tendo la kuwa na adabu ni silaha katika jamii yoyote ile. Kuwa na adabu ni ishara ya malezi bora mtu anayoyapata kutoka kwa wazazi wake. (BAKITA, 2015). Adabu ni kipengele kimojawapo cha Ontolojia ya kiafrika ambapo



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
ISSN: 2663-9289
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

humfanya mtu aweze kukubalika katika jamii anamoishi. Aidha, kwa Waafrika, tendo la adabu ni nguzo katika maisha ambayo huwasaidia wanajamii kuepuka matatizo mbalimbali yanayotokea katika jamii. Katika tamthiliya hii, suala la adabu limesawiriwa kama jambo muhimu linaloonyesha uzuri wa mtu. Watoto wanajukumu la kuwasalimia wakubwa kwa adabu na kuwasikiliza. Katika kusawiri tendo la adabu mwandishi anamwonyesha mhusika Juma jinsi anavyo onyesha adabu kwa mama Kitaru. Anasema:

> **Juma:** *Shikamoo.*
> **Mama:** *Marhaba, marhaba mwanangu. Pita; unasitasita nini? (uk. 13).*

Kwa hivyo, kitendo cha Juma kuonyesha adabu kwa mama Kitaru kinamfanya mama Kitaru ajisikie fahari ya kuwa mama na kumuona Juma kama mwanawe. Aidha, kwa Waafrika mtu yoyote anapokuwa na adabu njema katika jamii yake anajijengea tabia ya kupendwa na Mungu pamoja na watu wote wanaomzunguka.

**viii. *Suala la Utu***

Katika jamii za Waafrika suala la utu ni kipengele muhimu sana. Katika nadharia ya Ontolojia inasisitiza suala la utu kwa sababu katika mhimili wa nadharia hii unaamini kuwa Mungu aliwaumba wanadamu ili waishi kwa upendo na kuthamini utu wa kila mmoja katika jamii. Utu ni mwenendo au tabia ya kujali na kuthamini maisha ya binadamu (BAKITA, 2015). Waafrika wanaamini kuwa mtu hawezi kukamilika bila wengine, ndiyo maana utu huwa na uzuri wa namna mbalimbali kama kutatua matatizo ya wanajamii na kusuluhisha migogoro.

Abdulhamid na Baruwa (2016) wanasisitiza kuwa hukumu kuhusu uzuri au ubaya wa mtu itolewe kwa kujiegemeza katika kiwango cha utu wa mtu husika. Naye, Maganga na Mrope (2015) wanaona kuwa kila binadamu ana utu wandani na utu wa nje, utu wa ndani unaweza kuwa imara kuliko utu wa nje, na utu wa nje unaweza kuwa imara kuliko utu wa ndani. Katika tamthiliya ya *Mashetani* imesawiri suala la uzuri wa utu. Tamthiliya hii inaonyesha namna utu unavyowafanya watu waoneane huruma. Katika kusawiri hoja hii inathibitika kama ifuatavyo;

> **Binadamu**: *Binadamu wenzangu wote watanionea huruma. Watasema: Maskini Hawezi kutulia. Balaa imempata, ameingiwa na mashetani. Wanamtesa, wanamdhulumu. Afanyeje maskini naye hana uwezo wa kupambana na mashetani. Kuna binadamu akaweza kupigana na shetani? (uk.11).*

Hoja hii inadhihirisha kuwa, kutokana na tabia ya utu walionao Waafrika tatizo la mwanajamii mmoja katika maisha yao huonekana ni tatizo la watu wote. Katika kuonyesha umuhimu wa jambo hili, tamthiliya ya *Mashetani* inaeleza kuwa endapo tatizo la mwanajamii lisipopewa kipaumbele na watu wengine katika jamii inayomzunguka, watu hao watakuwa wametenda tendo lisilokubalika kijamii.

**ix. *Matumizi ya Mhusika Shetani***

Kulingana na nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika mashetani ni kipengele cha Ontolojia. Katika mhimili wa nadharia ya Ontolojia Waafrika wanaamini juu ya mashetani kuwa waliumbwa na Mungu. Shetani ni kiumbe kisichoonekana kwa macho ya nyama lakini athari zake zinaonekana kulingana na matendo maovu anayoyatenda binadamu katika kumtendea binadamu mwenziwe. Katika tamthiliya ya *Mashetani* hali hii imeweza kudhihirika katika maisha ya Binadamu pale ambapo anajitahidi kujikwamua kujitoa katika hali ya maisha duni ili kuwa na maisha mazuri lakini jitihada zake zinaishia kugonga mwamba. Kwa mfano kisa cha majigambo ya mhusika Shetani kuwa uwezo wake ni alfa na omega yanaamsha ari ya Binadamu kutaka kupambana naye ili awe huru. Katika kudhihirisha dai hili Shetani anasema:

> *Unanijua mimi nani?*
> *Mimi Shetani*
> *Sio jini wala kuhani*
> *Mimi Shetani… (uk.01).*

Hivyo basi, nukuu hapo juu inadhihirisha kuwa mapambano dhidi ya Shetani na Binadamu bado



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ISSN: 2663-9289

yanaendelea na hivyo kuifanya jamii kuwa makini na mambo yanayopelekea migogoro ya wenyewe kwa wenyewe ili kuleta mshikamano wa kufanya kazi kwa pamoja na kuleta maendeleo yanayohitajika kwa jamii.

**x. *Suala la Malezi***

Kazi ya malezi katika jamii za Kiafrika ni jukumu la kila mmoja. Kwa mujibu wa TUKI (2004) neno malezi lina maana ya njia za ukuzaji wa mtoto kwa kutarajia kufuata tabia na mwenendo unaostahili. Utafiti huu ulibaini kuwa, mwanamke amejengwa na kuaminishwa na mfumo wa jamii kuwa kazi yake kubwa ni kulea familia na kukaa nyumbani. Katika tamthiliya hii suala la malezi limeangaziwa kama kipengele cha Ontolojia ya Kiafrika. Katika mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ontolojia unaeleza kuwa Mungu aliyewaumba wanadamu huwapa maarifa ya kuweza kuwalea watoto wao katika malezi bora. Katika jamii ya Waafrika suala zima la malezi kwa watoto mara nyingi linafanywa na mama ambaye muda wote yupo nyumbani. Katika tamthiliya hii mama yake Juma na mama yake Kitaru ndio wanao kuwa nyumbani wakiendelea na shughuli za nyumbani. Dai hili linadhihirishwa na mama yake Juma anapomkemea mtoto wake ili awe na tabia njema kama ifuatavyo:

> **Mama:** *Acha tumseme. Ukimfanya hivyo ndio anazidi kichwa. Anajidekeza kama nini kwako huyo. Kaharibika siku hizi kama nini. Siku ile hapa nili… (uk. 36).*

Katika nukuu hapo juu inaonyesha jinsi mama yake Juma anavyojitahidi kumlea mwanawe katika maadili mema ingawa anakutana na upinzani mkubwa wa Bibi ambaye alikuwa anamdekeza mjukuu wake lakini bado anajitahidi kumlea mtoto wake ili akue katika malezi mazuri na aweze kukubalika na jamii yake.

**2. Vipengele vya Ontolojia ya Kiafrika katika Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi***

Kwa kurejelea tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* (1990) ya S. Mohamed, mwandishi ametumia vipengele vya Ontolojia ya Kiafrika kwa kuonyesha mambo mbalimbali ambayo yanafanyika katika jamii za Kiafrika kama sehemu ya maisha yao ya kila siku kwa njia mbalimbali.

**i. Matumizi ya Nyimbo**

Waafrika huamini kuwa uwezo wa kuimba ni kipaji anachopewa mtu kutoka kwa Mungu. Katika nadharia ya ontolojia ya Kiafrika nyimbo ni kipengele kimojawapo kilichobainika katika tamthiliya hii ambacho Waafrika hukitumia katika shughuli mbalimbali. Msokile (1981) anafasili nyimbo kama mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalumu. (Wamitila 2002, Samwel 2013) wanaeleza kwamba nyimbo ni utanzu wa fasihi simulizi. Katika kuchambua tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* mtafiti aliweza kubaini kuwa, mwandishi ametumia nyimbo kama kipengele kimojawapo cha Ontolojia ya Kiafrika ili kudhihirisha kuwa Waafrika wanatumia nyimbo katika mambo mbalimbali. Kwa mfano katika tamthiliya hii mtangazaji anawaamrisha Wari wote waimbe ili kumkaribisha Bi. Kirembwe kama ifuatavyo;

> **Mwari I:** *Bi. Kirembwe…* (*Anaongoza wimbo*)
> **Wari wote:** *Aja… … aja… aja!*
> **Mwari I:** *Bi. Kirembwe… … … .*
> **Wari wote:** *Aja… … aja… aja! … (uk. 33).*

Dhima ya wimbo huu ulikuwa ni kumkaribisha Bi. Kirembwe ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye sherehe ya kuwaingiza Wari katika mji wa Giningi. Finnegan (1977) kupitia utafiti alioufanya kuhusiana na fasihi simulizi katika Afrika ameonyesha kuwa nyimbo huimbwa wakati wa kazi mbalimbali Kwa mfano; uwindaji, ukulima, pia nyimbo huimbwa wakati wa sherehe mbalimbali, kama vile harusi, mahafali, jando na unyago na kadhalika. Hivyo, nyimbo ni hazina kubwa kwa Waafrika ambayo huhifadhi na kusambaza mawazo juu ya maisha ya Waafrika na maendeleo yake.

**ii. Matumizi ya Mhusika Sauti**

Waafrika wanaamini juu ya mhusika sauti. Katika tamthiliya hii mhusika au wahusika wanaonekana wenye kauli moja kimamlaka dhidi ya watu wanaokwenda



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ISSN: 2663-9289

kinyume na maadili ya jamii. Senkoro (1982) anaeleza kwamba wahusika ni watu ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu katika kazi za fasihi. Wahusika wanaotumika katika tamthiliya wanatofautiana kwa namna fulani na wahusika wa kazi nyingine kama riwaya (Wamitila, 2003). Katika tamthiliya hii mhusika sauti wamesawiriwa kama kipengele cha Ontolojia ya Kiafrika ambapo katika mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ontolojia usemao kuwa Mungu muumbaji huwagawia wanadamu sauti ili wazitumie katika kukemea mambo maovu yanayotokea katika jamii. Haya yanathibitika kupitia nukuu ifuatayo;

> **Sauti**: *Ha, ha, haaaaaaa! (Sauti inaendelea kucheka) Hujawamshindi Bi. Kirembwe … Ushindi hauji kwa vitisho na nguvu … huo hauitwi ushindi huitwa varange …*
> **Bi. Kirembwe**: *Nani wewe?*
> **Sauti**: *Bora useme nini hicho?*
> **Bi. Kirembwe**: *Nini…ni nini hicho? (Kaemewa zaidi)*
> **Sauti**: *Sauti … (uk. 127).*

Hali hii inaonyesha kuwa, Waafrika huamini katika sauti za watu waliokwisha kufa kwa sababu huweza kuwasiliana na watu walio hai katika kuwaelekeza jambo zuri au kuonya kuhusu jambo baya. Katika tamthiliya hii sauti za mizimu zinasikika zikikemea maovu yatokanayo na utawala mbovu wa Bi. Kirembwe dhidi ya watu anaowaongoza. Sauti hizo ni za watu ambao kivuli chao bado kinaishi hata sasa ili kutetea maslahi ya watu wengine wanaoonewa kutokana na nguvu za mamlaka.

**iii. Matumizi ya Mdundo wa Ngoma**

Utafiti huu umebaini kuwa Waafrika wanaamini juu ya matumizi ya mdundo wa ngoma. Imani hii inadhihirika kutokana na masuala mbalimbali ya kiutamaduni yanayofanyika katika jamii. Utanzu wa ngoma za kifasihi huhusu ngoma zinazotoa kauli za kimapokeo kwa ajili ya kuitahadharisha jamii, kuiarifu jamii, kuwafanya wanajamii kuwasiliana (Samuel, 2013). Kwa kuongozwa na misingi ya nadharia hii Waafrika wanaamini uwepo wa Mungu ambaye huwapa maarifa ya kutumia vifaa walivyonavyo kwa lengo la kuwasaidia kuelewa jambo fulani. Katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* mwandishi ametumia ngoma kama kipengele cha Ontolojia ya Kiafrika katika maonyesho tofauti tofauti na kwa malengo tofauti. Kwa mfano katika tamthiliya hii mlio wa ngoma umeonekana kama njia mojawapo ya kuonyesha kufahamu na kuutambua utawala wa Giningi na maisha yote ya Giningi. Kwa mfano anaposema;

> **Bawabu 1:** *A-a, ngoja kwanza. Ngojea mlio wa ngoma wendenao: ufuatane nao. Mlio wa ngoma unakuja; kwanza kidogo kidogo halafu unarindima kwa nguvu… (uk.13).*

Nukuu hii ni ishara kuwa Waafrika wanaheshimu na kuzikumbatia mila na desturi zao katika kudhihirisha utamaduni wao na jinsi ya kuongoza maisha yao ya kila siku kwa kutumia vitu walivyo navyo. Vipengele hivi vya Ontolojia ya Kiafrika vinatuonyesha na kutudhihirishia kuwa utunzi wa tamthiliya huipa fasihi ya Kiswahili sifa ya kukubalika miongoni mwa wasomaji ambao chimbuko lao ni Afrika.

**iv. Suala la Uchawi na Uganga**

Katika nadharia ya Ontolojia neno uganga katika jamii ya Waafrika lina ashiria taaluma ya tiba na uponyaji. Kulingana na Kim, tafsiri kuhusu uganga inatoa picha ya matibabu na tiba ya mwili au kisaikolojia, ilhali uganga hushughulika na utabiri wa kibinadamu kikamilifu zaidi kuliko kushughulikia matibabu (Kim 2010). Katika mihimili ya nadharia hii ipo nguvu ya Mungu ambaye huwapa wanadamu uwezo wa kuponya kupitia nguvu za uganga. Uganga ni taasisi inayochanganya dini, uchawi, afya na kuleta mizozo kati ya watu katika aina moja ya imani na mazoea ya kitamaduni (Erdtsieck 2003). Waafrika wanaamini juu ya uchawi na uganga ambapo katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* mbinu hii imetumika kwa lengo la kuionyesha hadhira ujanja wa tabaka tawala katika kuhakikisha kuwa wanabaki madarakani muda wote bila kujali namna watawalavyo. Kwa mfano Bi.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Kirembwe anajinadi kwa maneno ya kujiamini anaposema;

> *… Aaaa, bado unataraji mimi nikae kimya… juhudi zangu za kuwafunga kwa makafara na sihiri kubwa kubwa… (uk. 110).*

Mwandishi anaonyesha kuwa jambo hili la uchawi na ushirikina ni jambo la kawaida kwa Waafrika kwa sababu lina nafasi yake na wakati maalumu na wakati huo ukiisha halina nguvu tena.

**v. Suala la Mizimu**

Utafiti huu umebaini dhana ya mizimu kama kipengele kimojawapo cha Ontolojia ya Waafrika. Tempels (1959) anabainisha kuwa, katika Ontolojia ya Kiafrika kuna uhusiano kati ya mizimu na watu walio hai, hivi kwamba majanga yanapotokea jamii huomba kwa mizimu ili kuweza kupata ufumbuzi wa matatizo yao. Aidha, Waafrika hufuata mawazo ya mizimu na huamini kuwa kama mizimu ikikosewa huweza kutoa adhabu kwa wanaoishi, lakini ikitendewa vizuri huleta amani na mafanikio katika jamii. Katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* Mtolewa anasikia sauti na kutambua kuwa ni ya mizimu. Dai hili linadhihirika katika nukuu ifuatayo;

> **Sauti**: Mtolewa……*Mtolewa baba…Mtolewa mtoto wetu……Mtolewa…*
> **Mtolewa:** *Naam…… (Anaitika usingizini)*
> **Sauti:** *Mtolewa unatusikia lakini?*
> **Mtolewa:** *Nakusikieni……nakusikieni… (uk. 84).*

Nukuu hii inatuonyesha kuwa, katika jamii za Kiafrika mizimu au wahenga ni sehemu ya maisha yao kwa kuwa mtu anapokufa huwa na uwezo wa kuwasiliana na watu walio hai katika mambo mbalimbali. Kutokana na nadharia ya Ontolojia kupitia misingi yake imesaidia kugundua kuwa katika dini ya Kikristo waamini husali kupitia kwa watakatifu mbalimbali ili kufikisha shida zao kwa Mungu na hivyo kufanya muunganiko kati ya Mungu na watu wake waliopo duniani.

**vi. Matumizi ya Ardhi**

Ardhi ni kipengele kimojawapo cha Ontolojia kinachotambulika kama chanzo cha uhai wa mwanadamu. Katika msingi wa nadharia hii ya kuwepo, Waafrika wanaamini kuwa binadamu wa kwanza aliumbwa kwa udongo na kuwa kiumbe hai. Katika ardhi mwanadamu hujishughulisha katika shughuli mbalimbali ili kujipatia mahitaji yake ya msingi kama vile chakula, hewa safi kutokana na miti, maji, makazi ya kuishi na kadhalika. Perrinder (1967) anaeleza kuwa ardhi ni sehemu yote iliyo juu na chini ya uso wa nchi, vitu vyote vyenye kuota kiasili juu ya nchi, majengo na miundo mingineyo iliyojitokeza kwa kudumu juu ya ardhi. Katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* kipengele hiki kimehusika pale ambapo mkulima alipokuwa akiingia Giningi alitakiwa kuleta chakula cha kutosha kwa ajili ya wananchi wote wa Giningi lakini akaleta chakula kidogo kutokana na ukosefu wa pembejeo za kutosha. Kipengele hiki kinadhihirika kama ifuatavyo;

> **Bawabu11**: *(Anakagua kipeto na kasha anaandika kwenye jalada lake alilolikamata mkononi). Ah- hivi hii ni kazi ya mwaka mzima? Ulikuwa ukifanya nini siku zote hizi? Unadhani mpunga huo unatosha Kwa hazina ya Giningi Hautoshi Kwa chakula chako, seuze kwa hazina kuu ya Giningi… (uk. 18).*

Hii inaonyesha kuwa ardhi ndio msingi mkuu wa uzalishaji mali yaani chakula kwa binadamu na viumbe hai wengine kwa sababu katika ardhi ndipo mwanadamu hujikita katika shughuli mbalimbali ili aweze kupambana na mazingira yake na hivyo kujipatia mahitaji yake ya kila siku.

**vii. Dhana ya Wakati**

Dhana ya wakati ni kipengele kingine cha Ontolojia ya Kiafrika kilichosawiriwa katika tamthiliya hii. Waafrika wanaamini kuwa Mungu ndiye anayeanzisha maisha ya mwanadamu na mwisho unapofikia hukoma. (Mbiti, 1969) anaeleza kuwa, jamii za Kiafrika zinaamini kwamba



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing
Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

maisha ya mwanadamu huanza na kuelekea mwisho. Naye Kezilahabi (1985) anaeleza kuwa, njia mojawapo ya kuondoa utata uliomo katika dhana ya wakati katika fasihi ni kugundua maana ya maisha yenyewe kwa sababu maisha yamo katika mzunguko. Katika kuchambua tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* dhana hii ya wakati imesawiriwa pale ambapo Bi: Kirembwe alipogundua kuwa muda wake unayoyoma baada ya kuona kuwa utawala wake unaanza kushambuliwa na kizazi kipya. Mwandishi anatueleza kuwa;

**Sauti Nyingi***:* *(Kutoka nje) Bi: Kirebwe… leo yamekwisha … kama yalivyo anzia, leo hakuna kizuizi… leo ndio ile siku yetu na yako… leo ndio leo… tunakuja ndani, hakuna uchawi, hakuna ulinzi… (uk. 127-129).*

Hali hii inaonyesha kuwa, kila jambo na wakati wake. Wakati unapofikia wa kutenda jambo fulani ni lazima jambo hilo litendeke na ndio maana wakati wa Bi: Kirembwe unafikia tamati baada ya Mtolewa kutii sauti ya wahenga na kuchukua jukumu la kuwanywesha wari unga wa rutuba na ndipo wakaweza kutambua haki zao. Hivyo basi, maisha ya mwanadamu huongozwa na wakati na wakati unapotimia hakuna kipingamizi chochote cha kuweza kuzuia jambo fulani lisitendeke.

**viii. Matumizi ya Miviga**

Utafiti huu umebaini kuwa Waafrika wanaamini juu ya matumizi ya miviga. Msingi wao wa kuamini juu ya matumizi ya miviga umeegemea katika nadharia ya Ontolojia ambapo Waafrika hufanya sherehe mbalimbali zinazohusu utamaduni wao kama vile jando na unyago. Samwel (2013) anaeleza kuwa jando na unyago kwa kawaida huenda pamoja. Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* ni mfano mzuri wa matumizi ya miviga, hali hii imejitokeza pale ambapo Wari wa kike na wa kiume pamoja na Mtolewa wanapoingizwa mbele ya kiti cha enzi cha Bi. Kirembwe na kupewa unga wa ndere ili wabadilishwe daraja walilokuwamo na kukubalika katika jamii ya Giningi. Katika kuthibitisha dai hili mwandishi anaeleza kama ifuatavyo; Bi. Kirembwe anawaita wari:

**Bi. Kirembwe:** *Mwari wa kwanza njoo… (Mwari anasogea kwa Bi. Kirembwe kwa kutambaa kwa miguu na mikono- anasita karibu yake Bi. Kirembwe akichota unga wa ndere) Fungua kinywa (Anammiminia kinywani) Rangi gani hii? (anamwonyesha rangi nyeusi).*

**Mwari I**: *Nyeupe … (uk. 48-49).*

Baada ya Wari wote kulishwa unga wa ndere na kuonekana kuwa wamefuzu mafunzo ya kuingia katika kundi la watii na wafuasi wa Giningi kama ilivyohitajika, walikubaliwa kuitumia Giningi na kuitumikia kulingana na taratibu zilizowekwa chini ya utawala wa wa jadi wa Bi. Kirembwe. Hali hii inadhihirisha kuwa jamii za Kiafrika hufanya miviga katika shughuli mbalimbali kulingana na jamii husika.

**ix. Suala la Methali**

Utafiti huu umebaini kuwa methali kwa jamii za Waafrika ni kitu muhimu sana chenye kubeba hekima kwa jamii iliyopo na kizazi kijacho. Kulingana na nadharia ya Ontolojia katika msingi wa Mungu muumbaji ambaye huwapa wanadamu uwezo wa kuitumia hekima hii iliyobebwa na methali ili kuifanya jamii kuishi katika maadili yanayokubalika. Methali ni semi fupi zinazo sheheni fumbo juu ya ukweli wa maisha ya binadamu (Simiyu, 2011). Methali huwa na lugha teule iliyofumbata sitiara, nidaa, tashbihi, taswira, maswali ya balagha, takriri, mchezo wa maneno, tamathali za semi, tanakali sauti na mbinu za kinudhuma. Kwa hivyo methali ndio sifa za Kiafrika zinazobeba hekima iliyofichama ndani yake. Katika tamthiliya hii mwandishi anathibitisha dai hilo katika ukurasa wa sita kama ifuatavyo:

**Mtoto v:** *Kwani hamjui nyiye kwamba Bi: Kizee ana maarifa? Chambilecho wazee, Kuishi kwingi kuona mengi na kujua mengi pia.*

Pia katika ukurasa wa ishirini na nne (24) ipo methali isemayo *"Unachumia juani kuja kula kivulini"* na katika ukurasa wa (111) ipo methali *"Majuto hakika ni mjukuu"*.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Hali hii inaonyesha kuwa kwa Waafrika suala la methali ni hazina kwa vizazi vijavyo. Hivyo kipengele cha methali hudhihirisha uontolojia wa Waafrika katika kubeba hekima ambazo husisitiza jamii kuwa na maadili mema. Kwa ujumla utafiti huu umeweza kubaini kuwa katika jamii za Waafrika kipengele cha methali husaidia sana kukuza maarifa ya kuweza kufanya jambo lolote kwa bidii na uangalifu mkubwa ili mwisho wa jambo hilo mafanikio yaweze kupatikana.

**x. Suala la Umoja na Mshikamano**

Umoja na mshikamano ni kipengele cha Ontolojia ya Kiafrika ambacho kimejitokeza katika tamthiliya hii. Utafiti huu ulibaini kuwa umoja na mshikamno ni jambo muhimu sana katika jamii za Kiafrika. Jamii inapokuwa katika hali ya umoja ni rahisi sana kuwa na maendeleo chanya kwa kila jambo wanalolifanya ndio maana wahenga walisema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kulingana na nadharia ya Ontolojia katika msingi wake wa Mungu muumbaji ambaye huwapatia wanadamu uwezo wa kufanya jambo fulani kwa umoja na mshikamano kati yao na matokeo yake ni kupata mafanikio chanya. Katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* hali hii ilionekana pale ambapo Mtolewa alisisitizwa na wahenga aende kuwakomboa wari waliokuwa chini ya uongozi mbaya wa Bi; Kirembwe. Nukuu ifuatayo inathibitisha dai hili;

> **Mwari 1**: *Nyeupe ni nyeupe na nyeusi ni nyeusi… na nyekundu ni nyekundu, nyekundu haiwezi kuwa manjano … (uk. 103).*

Hali hii ya mabishano imejitokeza baada ya Mtolewa kushirikiana na wahenga pamoja na wari. Kitendo cha wari kukubali kulishwa unga wa rutuba kimeonyesha umoja waliokuwa nao na ndipo wakaweza kujipatia uhuru wao nje ya utawala wa Bi: Kirembwe. Hivyo, katika jamii za Kiafrika kufanya mambo kwa kushikamana ni jambo lenye tija kwani huwawezesha kupata maendeleo kwa pamoja na sio mtu mmoja mmoja.

**xi. Suala la uzazi**

Waafrika wanathamini sana suala la uzazi kwa sababu kutokana na nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika kupata watoto ni baraka na ugumba ni laana. Kulingana na nadharia hii katika msingi wake wa Mungu muumbaji ambaye huwapatia wanadamu uwezo wa kuzaa watoto wengi kunaonekana kuwa ni baraka katika familia na jamii kwa ujumla. Katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* tunaona jinsi wahenga walivyothamini uzazi kwa kumsihi mtoto wao Mtolewa awe chanzo cha kuwasaidia wenzake waliokuwa wakionewa kutokana na utawala mbaya wa Bi. Kirembwe. Kwa mfano katika tamthiliya hii mwandishi anaeleza kama ifutavyo;

> **Sauti:** *Unatambua? Unatambua kwamba wewe ni mtoto wetu? Unatambua kwamba wewe sisi ndio tulio kuzaa? Tulikuvyaza kwa utonvu unaotoka kwenye nyuti za migongo yetu … (uk. 85-86).*

Nukuu hapo juu inadhihirisha jinsi Waafrika wanavyothamini uzazi na kuona kuwa ni jambo la muhimu sana na ndio maana wahenga wanamhimiza mtoto wao Mtolewa kufanya jambo la kuwaokoa wari mikononi mwa utawala dhalimu wa Bi: Kirembwe. Kwa Waafrika suala la uzazi ndio mwendelezo wa maisha hapa duniani na tendo la kuweza kukumbukwa baada ya maisha ya hapa duniani.

**Hitimisho**

Makala haya yamejadili namna vipengele vya Ontolojia vinavyochangia kuipa tamthiliya ya Kiswahili sura ya Uafrika. Mjadala umebaini hilo kwa kuzichambua tamthiliya za Kiswahili ambazo ni *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*, aidha mjadala huu umethibitisha kuwa vipengele vilivyobainishwa katika tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* vimesawiri maisha ya Kiafrika kwa ujumla na kuwajengea Waafrika uwezo wa kujiamini na kuamini vitu walivyonavyo kuliko kutegemea uwezo wa watu kutoka magharibi.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268
Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|
Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org
Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

ISSN: 2663-9289

## MAREJELEO

Abdulhamid, M. na Baruwa, A. (2006). *Methali za Kiswahili*: *Maana na Matumizi*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezirahabi Katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu*. Tasnifuya Shahada ya Uzamifu. (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Duwe, M. (2016). "*Mdhihiriko wa Falsafa ya Uduara katika Sanaa za Maonesho za Jamii ya Wangoni*" Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Erdtsiek, J. (2003). *In the Spirit of Uganga.* Inspired Healing and Healership in Tanzania. Amsterdam: Universiteit van Amsterdam, AGIDS.

Finnegan, R. (1977). *Oral Poetry*. Nairobi: Combridge University Press.

Geofrey, P. (1969). *Religion in Africa*. Canberra: Penguin Books.

Heidegger, M. (1999). *Ontology-The Hermeneutics of Facticity*. India: Indiana University Press.

Hussein, E. (1971). *Mashetani.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Kajosi, S. (2013). "*Suala la Uzazi katika Ontolojia ya Kibantu na Jinsi Lilivyojitokeza katika Riwaya ya Kiawahili*". Tasnifu ya Shahada ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (1985). *African Philosophy and the problem of Literary Interpretation.* (Tasnifu ya Umahiri). University of Wisconsin- Madison. (Haijachapishwa).

Kiango, S. D. (1973). "*Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili Upande wa Michezo ya Kuigiza" katika Kiswahili.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI. 43:2:88-96.

Kim, C. (2010). *Jinn Possession and Uganga (Healing) among the Swahili*: A Phenomenological Exploration of Swahili Experience of Jinn. Muslim-Christian Encounter 5: 67-88.

Maganga, M. na Mrope, M. (2015). *Kila Binadamu Ana Utu wa Ndani na Utu wa Nje* (Shetani Hana Maslahi na Umaskini). magangameshack.blogspot.co.ke/2015/09.

Mbiti, J. S. (1969). *Introduction to African Religion*. Heinemann: University of Michigan.

Mbiti, J. S. (2011). *African Religion and Philosophy*. Kampala: East African Educational

Mbogo, E. (2008). *Ngoma ya Ng'wana malundi*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Mohamed, S. A. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Oxford University Press, Nairobi.

Msokile, M. (1981). *Nafasi ya Nyimbo za Fasihi simulizi katika Jamii Iliyomdikwa*. Makala za Fasihi simulizi Chuo Kikuu Cha Dar-es –Salam.

Omari, S. (2009). "*Hip Hop Music as Popular oral Poetry*." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Nyanto, S.S. (2016). "*Religious Experiences of Life after Death in Buha and Unyamwezi Cosmologies, Western Tanzania.*" In History Research. Juz. 6 Na. 2, kur. 80-100.

Parrinder, G. (1967). *African Traditional Religions*. London: Sheldon Press.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

**Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)**

**ISSN: 2663-9289**

**DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.268**
**Volume: 03 Issue: 01 | Sep-2021|**
**Received: 18.09.2021; Accepted 20.09.2021; Published on 30.09. 2021 at www.editoncpublishing.org**
**Karata, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal***

Roe, C. (2012). *A Short History of Ontology*. Iliyosomwa tar. 18.08.2017 Katika www.daraversity. net/a-short- history-of-ontology.
Salem, S. (2013). *Maudhui na Fani katikaTamthiliya za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Mashetani na Kivuli Kinaishi.* Tasnifu ya Uzamifu katika Kiswahili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa). Dares Salaam, Tanzania.
Samwel, M. (2013) *Tamthiliya ya Kiswahili; Kutoka Miviga ya Kidini hadi Filamu;* Dar es Salaam; Mevelli Publishers.
Senkoro, F.E. M. K. (1982). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu Cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*, Mwanza: Serengeti Bookshop.
Smith, B. (2003). "*Ontology*". Katika L. Floridi (Mh.), Blackwell Guide to the Philosophy of Computing and Information. Oxford: Blackwell. Kur. 155–166.
Stumph, S. E. na Fierser, J. (2008). *Socrates to Sartre and Beyond a History of Philosophy*. New York: Mac Graw-Hill Company.
Temples, P. (1959). *Bantu Philosophy*. In the Titi Turdorancea bulletin. Paris: Presence Africaine.1991-2011.
Tuki, (2004). *Kamusi ya Kiwsahili Sanifu*. Oxford University Press, East Africa Ltd.
Wamitila K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
Wamitila K.W (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publisher.
Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Focus Publication Ltd. Nairobi Kenya.



**© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org**